**Taarifa kwa Vyombo vya Habari:** 21 Desemba 2009

Kwa Mawasiliano: Prof. Jamidu Katima, 0754 265864

---

# Utafiti wa kwanza wa rangi wabaini kuwepo kwa madini ya risasi katika rangi kwa 77%

## Rangi zilizopo kwa wingi katika soko ni za aina ya Goldstar, Sadolin na Coral

## *Watoto wapo hatarini kuathirika na sumu hizo; rangi salama zinapatikana*

Utafiti wa rangi zitumikazo katika kupaka nyumba na vifaa vinginevyo zinazouzwa jijini Dar es Salaam na kwingineko nchini uneonesha rangi hizo kuwa na kiasi kikubwa cha madini ya risasi (lead). Utafiti huo uliohusisha sampuli 26 za rangi, umeonesha kuwa sampuli zote 26 (100%) kuwa na madini hayo. Rangi zote za mafuta zilionesha kuwa na kiasi kikubwa cha madini hayo kuzidi kiwango kinachoruhusiwa katika rangi nchini Marekani, wakati rangi zote za maji zilionekana kuwa na kiwango kidogo cha madini ya risasi chini ya kile kinachoruhusiwa nchini Marekani (yaani sehemu 90 ya milioni – 90 ppm). Utafiti huu unaaminiwa kuwa wa kwanza wa aina yake nchini Tanzania.

Matokeo halisi ya utafiti wenyewe ni kama ifuatavyo:

- Utafiti ulihusisha sampuli 20 za rangi za mafuta kutokana na aina 3 za kampuni za rangi, yaani Goldstar, Sadolin na Coral
- 100% ilizidi kiwango cha madini ya risasi kinachoruhusiwa nchini Marekani (sehemu 90 ya milioni)
- 95% ilizidi kiwango cha sasa cha madini ya risasi kinachoruhusiwa nchini Tanzania yaani (sehemu 90 ya milioni).
- Aina za rangi zilizokuwa na viwango vya chini ya viwango vya nchini Marekani vya madini hayo ni sampuli zote za rangi ya maji za Goldstar (mist pink, summer blue), Coral (summer blue, candy pink) na Sadolin (mist pink, summer blue).

Madini ya risasi yanasababisha kuharibika kwa mfumo wa fahamu kiasi cha kutoweza kutibika tena na kupungua kwa ufahamu hata kiasi cha madini hayo kikiwa kidogo. Madini hayo yanahusishwa zaidi na athari kwa watoto wadogo kiasi cha kuwafanya kuwa wazito au kutoweza kutamka maneno mbalimbali na uelewa katika kulinganisha maandishi tofauti, uthabiti katika kufuatilia mafunzo na mawasiliano madogo kati ya macho na mikono katika kufanya kazi kama kuandika na hivyo matokeo mabaya katika masomo, shukeni. Kwa sababu hizo madini ya risasi kwenye rangi yaliishapigwa marufuku nchi ngingi zilizoendelea kuanzia miaka ya 1920.

Mamlaka inayohusika na uhifadhi wa Mazingira nchini Marekani (U.S. EPA) imeweka madini ya risasi katika kundi la kemikali zinazoweza kusababisha saratani (kansa). Kulingana na Mfungamano wa Afya na Mazingira wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO Healthy Environments for Children Alliance), "*hakuna kiwango salama cha madini ya risasi katika damu, bali inafahamika kuwa madini hayo yanaongeza wigo, dalili na athari zake*

*pia."* Moja kati ya vyanzo vikubwa vya madini ya risasi kwa binadamu ni vumbi litokanalo na rangi zenye madini hayo zinapotumika, kuchakaa au kuoza. Madini hayo yanaweza kumuingia na kumuathiri mtu kupitia mdomoni na hasa kutokana na mikono iliyogusa au kushika madini hayo.

Mwaka 2002, taarifa ya Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO's *World Health Report)* ilianisha madini ya risasi kama moja ya njia ishirini za hatari zinazoathiri afya na vyanzo vya magonjwa, na kueleza kwamba, asilimia 40 ya watoto wana viwango vya madini ya risasi katika damu zao kwa kiwango cha juu (zaidi ya 5 µg/dl), na asilimia 97 ya watoto waliothirika wakiwa wanaishi katika nchi zinazoendelea.

*"Madini ya risasi yanatishia maendeleo ya kukua kwa ubongo (ufahamu) naafya kwa ujumla,"* anasema Daktari Rongo LMB wa Idara ya Afya ya Mazingira na Kazini ya Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba Muhimbili. *"Athari zitokanazo na madini hayo kwa watoto lazima zichukuliwe kwa tahadhari na umakini mkubwa, na wazazi lazima waelewe vyanzo vya watoto kuathirika na madini hayo ikiwa ni pamoja na rangi wanazotumia kupaka nyumba zao."*

*"Madini ya risasi ni sumu na lazima yaondolewe katika rangi na vitu vingine ambavyo watoto wanavitumia au kukutana navyo,"* anasema Dk. Vera Ngowi wa TAPOHE (asasi ya Afya ya Jamii, Kazini na Mazingira Tanzania -- Tanzania Association of Public, Occupational and Environmental Health Experts). *"Bara Ulaya walipiga marufuku matumizi ya madini ya risasi katika rangi katika miaka ya 1920. Tunasubiri nini wakati rangi mbadala na salama inapatikana? Tunataka kulinda watoto wetu kwa kuondoa madini ya risasi katika rangi."*

Utafiti huu umekuja wakati mahsusi ambapo kuna makubaliano na dhamira duniani kote ya kuondoa matumizi ya madini ya risasi katika rangi kwa nchi zote. Mwezi Mei 2009, wakati wa Mkutano wa Pili wa Kimataifa kuhusu Usimamizi wa Kemikali (International Conference on Chemicals Management), Tanzania ilikuwa miongoni mwa zaidi ya nchi 100 zilizopitisha Makubaliano ya kuondoa matumizi ya madini ya risasi katika rangi.

Kwa kushughulikia tatizo hili la madini ya risasi, Shirika la AGENDA la Mazingira na Maendeleo (AGENDA for Environment and Responsible Development - AGENDA) kwa kushirikiana na Mtandao wa Kimataifa wa Kuondoa Kemikali zisizooza (persistent organic pollutants - POPs) ujulikanao kama IPEN na Asasi isyoyo ya kiserikali Toxics Link la India, wamezindua kampeni ya kimataifa ijulikanayo kama "Afya ya Watoto Kwanza: Ondoa madini ya risasi katika rangi" (***"Children's Health First: Eliminate Lead Paint")*** inayolenga kuondoa madini ya risasi katika rangi na kuhamasisha matumizi ya rangi mbadala zisizo na madini hayo, kupitia Makubaliano ya Kimataifa ya kuondoa matumizi ya madini ya risasi katika rangi chini ya Mkakati wa Kimataifa wa kuelekea usimamizi salama wa kemikali (Strategic Approach to International Chemicals Management - SAICM).

*Kwa taarifa zaidi angalia tovuti ya kampeni hiyo kupitia:*

http://www.ipen.org/ipenweb/work/lead/lead_paint.html,
http://www.ipen.org/ipenweb/work/lead/lead_paint.html#fact

*AGENDA for Environment and Responsible Development (AGENDA) ni Shirika lisilo la Kiserikali (NGO) lililosajiliwa mwezi Julai 1997 na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi chini ya Sheria ya vyama vya hiari ya 1954 [Cap.337 (iliyorekebishwa)] likiwa na namba ya usajili SO.NO.9108 na baadaye namba ya kuridhia sheria mpya ya 2002, (compliance certificate) cheti namba 1518 cha 2005. AGENDA inahamasisha kila mwananchi kujenga utamaduni wa kuyajali na kuwajibika kwa mazingira kupitia shughuli za utetezi (advocacy), ujengaji wa uwezo na ushirikishaji wa wadau ndani na nje ya Tanzania (www.agenda-tz.org)*

---

*The International POPs Elimination Network (IPEN) ni mtandao wa mashirika ya kijamii, yasiyo ya kiserikali (NGOs) duniani wenye wananachama washirika zaidi ya 700 kutoka zaidi ya nchi 100 kutoka mabara yote. IPEN inafanya kazi na NGOs duniani kote kuelekea dunia salama kutokana na athari za kiafya na kimazingira zinazosababishwa na kemikali za sumu. www.ipen.org*

---

CHILDREN'S HEALTH FIRST

ELIMINATE LEAD PAINTS!